

**CHIMBUKO LA LUGHA TANDAWAZI KUTUMIKA KATIKA KISWAHILI
SANIFUNA ATHARI ZAKE KWA JAMII**

MILA SALUM ABDALLAH

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUPATIA SHAHADAYA UZAMILI YAKISWAHILI (M.A. KISWAHILI
FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2018

UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo:
*Chimbuko la Lugha Tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu na Athari zake
kwa Jamii* na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili
ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu
Huria Cha Tanzania

.....

MOHAMED OMARY

(Msimamizi)

Tarehe.....

HAKIMILIKI

Haki zote za kunakili, kuiga au kuchukua sehemu ya tasnifu hii zimehifadhiwa kisheria. Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kunakili au kuiga tasnifu hii bila idhini yangu au kibali cha maandishi kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

IKIRARI

Mimi *Mila Salum Abdalla* nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kinginekwa ajili ya Digirii yoyote.

.....

Saini

Tarehe.....

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazee wangu wapendwa na watu wote wa familia yangu kwa kuniunga kwao mkono katika masomo yangu ya ngazi zote.

SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyeezi Mungu Muumba wa mbingu na ardhi kwa kunijaalia uhai, uzima, na kunipa uwezo wa kufanya utafiti, kuandika na kuikamilisha kazi hii. Pili napenda niwashukuru wote waliochangia kwa nmna moja au nyingine kukamilka kwa kazi hii. Hata hivyo si rahisi kuwataja wote kwa majina, ila ninapenda kuwashukuru wote nitakaowataja na ambao sijawataja kwa mchango wao wa kuifanikisha kazi hii.

Shukrani za pekee ziende kwa msimamizi wangu, Mwa Bakari Kombo Bakari, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu na kunihimiza kufanya kazi kila alipohisi kuwepo kwa uduwazi na namna fulani ya kusita na kuchelewesha kazi. Yeye alikuwa kwangu ni mshauri, muelekezaji na mwalimu aliyenikosoa kwa busara na hekima kubwa kila ilipobidi kukosolewa na kuelekezwa. Cha kumlipa sina, lakini sitoacha kumuomba dua kwa Mwenyeezi Mungu amzidishiye moyo wa upendo na ampe nguvu aweze kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kwa manufaa ya sasa na baadae, ili wanufaike wengi wa enzi hizi na zijazo.

Shukrani zangu maalum ziwaendee wazazi wangu wapendwa; babangu na mamangu kwa mapenzi yao na huruma kubwa zilizowapelekea kunilea kwa uangalifu mkubwa na kunisomesha hadi kufikia elimu ya juu. Nitakuwa mwizi wa shukrani na mchawi wa fadhila iwapo nitawacha kuwashukuru wake watu wote wa familia yangu kwa kuniunga mkono katika masomo yangu.

IKISIRI

Kazi hii ilihusika na *Chimbuko la Lugha Tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu na Athari zake kwa Jamii*. Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili ambayo ni kuelezea chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu na Kubainisha athari za lugha tandawazi katika jamii. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa mbinu mbalimbali za utafiti zilihusika, ambazo ni hojaji, mahojiano pamoja na ushuhudiaji. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Nadharia kidhi ya mawasiliano (NKM) na Sampuli iliyotumika ni watu themanini (80), thelathini wataalamu wa lugha kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Wafanyakazi wapatao ishirini kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), pamoja na watoto 10, wazee 10 na vijana 10. Pia kulikuwa na mgawanyo sawia wa kijinsia, miongoni mwa makundi yote matano. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, mtafiti aligundua kwamba, Wazungumzaji wa lugha ndio chimbuko la lugha tandawazi kwani hutumia mitindo ya kuchanganya misimbo, huchanganya herufi na nambari na pia wanapotumiana ujumbe kwa njia ya simu huwa wanakata maneno na kudondosha irabu. Kundi kubwa linalotumia lugha tandawazi ni kundi la vijana wenye umri wa miaka 18-40 na wafanya kazi. Kuhusu athari za lugha tandawazi mtafiti amegundua kwamba lugha tandawazi ina athari za kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantikia. Mtafiti amependekeza mambo kadha na kuwaagiza watafiti wajao wayatupie macho na kuyafanyia kazi. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na Watumiaji wa lugha wajaribu kutumia lugha moja tu katika mawasiliano yao na wasichanganye misimbo ya lugha. Pia waache tabia ya kuchanganya maneno na nambari wakati wanapo tumiana ujumbe na waepuke kufupisha maneno kwa kudondosha irabu ili waoneshe uzalendo wao katika kukilinda na kukihifadhi Kiswahili kibakie kua sanifu.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	i
HAKIMILIKI.....	ii
IKIRARI	iii
TABARUKU	iv
SHUKURANI.....	v
IKISIRI.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ORODHA YA MAJEDWA.....	xi
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI WA UJUMLA	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.1.2 Maana ya Lugha na Lugha Tandawazi	2
1.2 Tatizo la Utafiti	3
1.3 Lengo la Utafiti	4
1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti	4
1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti.....	4
1.4 Maswali ya Utafiti.....	4
1.5 Umuhimu wa Utafiti	5
1.6 Hitimisho.....	5

SURA YA PILI.....	6
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA	6
2.1 Utangulizi.....	6
2.2 Dhana ya Lugha	6
2.3 Dhana ya chimbuko	7
2.4 Dhana ya Utandawazi	7
2.5 Lugha Tandawazi.....	7
2.6 Lugha ya Kiswahili na Usanifishaji	9
2.7 Kiswahili Sanifu.....	9
2.8 Pengo la Utafiti	10
2.9 Kiunzi cha Nadharia.....	10
2.9.1 Maana ya Nadharia	10
2.10 Hitimisho.....	12
SURA YA TATU.....	13
NJIA NA MBINU ZA UTAFITI	13
3.1 Utangulizi.....	13
3.2 Eneo la Utafiti	13
3.3 Sampuli na Usampulihaji.....	13
3.4 Usampulishaji	14
3.5 Watafitiwa/Kundi lengwa	14
3.6 Mbinu za Utafiti.....	16
3.6.1 Mbinu ya Ushuhudiaji.....	16
3.6.2 Mbinu ya Mahojiano.....	16

3.6.3	Mbinu ya Hojaji	17
3.7	Uchambuzi wa Data.....	18
3.8	Hitimisho.....	19
SURA YA NNE		20
UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ..		20
4.1	Utangulizi.....	20
4.2	Chimbuko la Lugha Tandawazi katika Lugha Sanifu.....	20
4.2.1	Tafsiri ya Matokeo kuhusu Chimbuko la Lugha Tandawazi.....	22
4.3	Uchanganyaji wa Lugha Mbili wakati wa Mawasiliano.....	25
4.3.1	Tafsiri ya Matokeo kuhusu Uchanganyaji wa Lugha Mbili wakati wa Mawasiliano	26
4.3.2	Lugha zilizochanganywa katika sampuli A	27
4.3.2.1	Mchanganyiko kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza	27
4.3.2.2	Mchanganyiko kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiarabu.....	27
4.3.2.3	Mchanganyiko wa Maneno na Nambari katika Uandishi.....	28
4.3.3	Tafsiri ya Matokeo kuhusu Mchanganyiko wa Maneno na Nambari katika Uandishi	29
4.3.4	Tafsiri ya Matokeo Matumizi ya Lugha Tandawazi kwenye Ujumbe wa Maandishikwa njia ya wasap kupitia Simu za mkononi	32
4.3.5	Tafsiri ya Matokeo kuhusu Lugha Tandawazi kwenye Kiwango cha Maneno	33
4.4	Kubainisha Athari za Lugha Tandawazi katika Kiswahili Sanifu	37
4.4.1	Athari ya Lugha Tandawazi kifonolojia (Kimatamshi).....	38

4.4.1.1	Tafsiri ya Matokeo kuhusu Maneno yaliyodondoshwa Baadhi ya Irabu....	40
4.4.2	Athari za Kisemantiki	41
4.4.2.1	Maana ya Semantiki.....	41
4.4.2.2	Utambuzi wa Maana ya Mfumo wa Lugha Tandawazi	43
4.4.3	Athari za Kimofolojia	44
4.4.4	Athari za Sintaksia	45
4.4.4.1	Tafsiri ya Matokeo kuhusu Athari za Sintaksia	46
4.5	Hitimisho.....	47
SURA YA TANO		48
HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO		48
5.1	Utangulizi.....	48
5.2	Muhtasari wa Utafiti	48
5.3	Matokeo ya Utafiti	50
5.4	Mchango wa Utafiti	50
5.5	Mapendekezo	51
5.6	Mapendekezo kwa Taasisi za kukuza na Kuendeleza Kiswahili.....	51
5.7	Mapendekezo kwa watumiaji wa Lugha.....	52
5.8	Mapendekezo kwa Vyombo vya Mawasiliano	52
5.9	Hitimisho.....	52
MAREJELEO		53
KIAMBATANISHO		57

ORODHA YA MAJEDWA

Jedwali na 3.1:	Jedwali la Mchanganuo wa Watafitiwa / Kundi Lengwa.....	15
Jedwali na 4.1:	Majibu ya Watafitiwa	21
Jedwali na 4.2:	Jinsia za Watafitiwa.....	23
Jedwali na 4.3:	Mifano ya Sentensi zilizochanganywa Lugha Mbili kwa Wakati Mmoja.....	25
Jedwali na.4.4:	Mchanganyiko wa Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kiingereza.....	27
Jedwali na 4:5	Mchanganyiko wa Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kiarabu ...	28
Jedwali na.4.6:	Mifano ya Sentensi zilizo changanywa Maneno na Nambari	28
Jedwali na.4.7:	Mifano ya Lugha Tandawazi wanayotumia Wazungumzaji wa Lugha katika Mazungumzo yao au kwa Njia ya Ujumbe katika Mawasiliano yao	30
Jedwali na 4.8:	Idadi ya watafitiwa wanaotumia Lugha ya Kiingereza na Kiswahili na wanao tumia Lugha ya Kiarabu na Kiswahili	32
Jedwali na. 4.9:	Lugha Tandawazi katika Kiwango cha Maneno	33
Jedwali na.4.10:	Maneno yenye Nambari hutamkwa kwa Kiswahili na Kiingereza.....	35
Jedwali na.4.11:	Utumiaji waLugha Tandawazi katika Kiwango cha Sentensi	36
Jedwali na. 4. 12:	Majibu ya Watafitiwa juu ya Athari ya Lugha Tandawazi	38
Jedwali na 4:13:	Mifano ya Maneno yaliyodondoshwa Baadhi ya Irabu.....	39
Jedwali na.4.13:	Mifano ya Matumizi ya Fonimu C Mahali pa Fonimu si katika Maandishi	40

Jedwali na. 4.14:	Linaloonesha jinsi Nambari zinavyotumika katika kuandika Maneno ya Lugha Tandawazi	41
Jedwali na. 4.15:	Maana ya (leksimu) yaliyoandikwa katika Mfumo wa Lugha Tandawazi	42
Jedwali na 4.16:	Maana ya (Tungo) zilizoandikwa katika Mfumo wa Lugha Tandawazi.....	43

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA UJUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii ni inahusiana na mada ya utafiti isemayo Chimbuko la Lugha tandawazi Kutumika katika Kiswahili Sanifu na Athari zake kwa Jamii. Utafiti huu utabainisha Chimbuko la lugha tandawazi pamoja na athari zake. Sura hii inakusudia kuainisha vipengele vya msingi vinavyohusiana na mada ya utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na Usuli wa Mada pamoja na Tamko la Utafiti. Vipengele vyengine vitakavyohusishwa na sura hii ni Malengo ya Utafiti, Maswali ya Utafiti, Umuhimu wa Utafiti pamoja na Mipaka ya Utafiti. Na mwisho sura itamalizia kwa kuelezea mipaka ya utafiti, na matatizo ya utafiti ambayo mtafiti wa utafiti huu anatarajia kukumbana nayo katika utafiti wake.

1.1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kiswahili ni lugha yenye idadi kubwa ya watumiaji. Watumiaji wake wanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni sitini upya. Lugha ya Kiswahili inazungumzwa takriban na kila mtu anaeishi nchini Tanzania na Kenya. Kuna watu zaidi ya milioni kumi na tano (15) katika nchi ya Demokrasia ya Kongo na baadhi ya sehemu za nchi za Rwanda, Burundi, Msumbiji, Malawi, Afrika ya kusini pamoja na nchi ya Uganda. Vilevile lugha ya Kiswahili inazungumzwa na baadhi ya nchi za arabuni kama vile Dubai na Omani. Pia kuna vyuo mbalimbali vinanyofundisha lugha ya Kiswahili, vilivyo ndani na nje ya nchi. Pia na kuna idhaa kadhaa ambazo zinatangaza kwa kutumia lugha ya Kiswahili za kitaifa na kimataifa.

Kutokana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili mnamo Mwaka 1925 na 1930 lugha ya Kiswahili ilisanifishwa na kuwa Lugha Sanifu. Wakati huo katika kisiwa cha Unguja kulikuwa na lahaja nyingi za lugha ya Kiswahili. Lahaja zilizokuwepo ni kama vile lahaja ya Kimakunduchi, lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kiunguja mjini. Lahaja zote hizo ziliangaliwa kwa makini zikachujwa na kupembuliwa kwa kina. Baada ya mjadala mkali na kutokana na umaarufu wake ukilinganisha na lahaja nyengine, lahaja ya Kiunguja mjini ilibahatika kuteuliwa na kuchaguliwa kuwa lahaja inayofaa kwa usanifishaji na hivyo Kiunguja mjini ndio lahaja inayotumika katika Kiswahili Sanifu. Mnamo mwaka 1967 serekali ya Tanzania ilitamka rasmi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa pamoja na lugha rasmi.

Lugha ya Kiswahili inakua kwa kasi ya ajabu (kubwa mno) lakini lugha hii inaathiriwa sana na utandawazi. Kwa hiyo lugha hii imesababisha mabadiliko makubwa na yalio mengi kimofolojia na hata kifonolojia. Maana ya lugha na lugha tandawazi imetolewa katika sehemu inayofuata:

1.1.2 Maana ya Lugha na Lugha Tandawazi

TUKI (1981) wanasema kwamba lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana. Mpangilio huu hutumiwa na watu wa taifa au kabila Fulani kwa ajili ya mawasiliano. Nayo kamusi ya Kiswahili (1990) inasema; lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ilil kuwasiliana. Nkwera (1979) anasema Lugha ni utaratibu (mfumo) maalum wa sauti za nasibu zenye maana ambazohutumiwa miongoni mwa binaadamu kwa madhumuni ya mawasilianomiongoni mwao. Sauti hizo ni lazima ziwe zakutamkika.

Kutokana na fasili za wtaalamu hawa ni dhahiri lugha ni mfumo wa sauti nasibu zilizobuniwa na binaadamu kwa ajili ya mawasiliano.

Kuhusu utandawazi Sweeting (1996) anasema kuwa; Utandawzi ni kuihusisha dunia ambayo ndiyo sayari mama na ndio maskani kwetu sisi ni kuona dunia kama kitu kimoja na watu wote ni wa kabila moja. Kwa mujibu wa Mutembei (2011), lugha tandawzi ni lugha inayotumiwa kwenye mitandao wakati wa kuandika ujumbe. Ni lugha yenye mchanganyiko wa maneno ambayo yana lugha zaidi ya moja na kuunda lugha tofauti. Lugha tandawazi ni lugha ya ufupisho ambao hupatikana kwa kudondosha baandhi ya sauti au kuchanganya maneno na nambari. Kwa mfano kusima100 = kusimamia, 2100 = tumia'. Kuna njia mbalimbali za mawasiliano yanayotumia lugha tandawazi. Miongoni mwa njia hizo ni kama vile simu, barua pepe na mitandao ya kijamii. Kutokana na kukua kwa utandawazi kumeibuka mitindo mipya ya utumiaji wa lugha kwenye mawasiliano na kusababisha athari kubwa katika Kiswahiji Sanifu na ndio maaana mtafiti katika eneo hili akahisi kuna haja ya kufanya uchunguzi makini kuhusu Chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili Ssanifu na Athari zake kwa Jjamii.

1.2 Tatizo la Utafiti

Kuna kazi mbalimbali za utafiti ambazo zimezungumzia juu ya lugha tandawazi. Baaadhi ya kazi hizo ni kazi ya Mutembei (kasha tajwa) ambaye alichunguza kuhusiana na simu za kiganjani. Lengo lake la msingi lilikuwa ni kuangalia matatizo yanayopatikana kutokana na utumiaji wa lugha tandawazi na athari zake. Craystal (2008) yeye alichunguza juu ya matumizi ya ujumbe mfupi na athari zake katika lugha ya Kingereza na maandishi yake.

Ogonda na wenzake (2011) wao waliandika juu ya vipengele vya sintaksia kwenye matini za ujumbe mfupi. Mohd (2013) nae alitafiti juu ya mtazamo wa wanafunzi na walimu kuhusu matumizi ya lugha tandawazi katika Kiswahili hasa wakati wa kuandika ujumbe kwenye simu za kiganjani. Ali (2016) alichunguza kuhusiana na athari za utandawazi katika lahaja ya Kitumbatu. Pamoja na jitihada kubwa zilizpofanywa na watafiti waliotajwa hapo juu, mtafiti wa utafiti huu kwa kiasi anachoelewa hajaiona kazi yoyote iliyofanywa yenye mada inayohusiana moja kwa moja na chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu. Kutokana na hali hii ndio mtafiti akahisi ipo haja ya kuchunguza chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu na athari zake kwa jamii ili kupunguza mwanya ulioachwa na watangulizi wake.

1.3 Lengo la Utafiti

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Katika utafiti huu lengo kuu ni kuchunguza chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu.

1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti

- i) Kuelezea chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu
- ii) Kubainisha athari za lugha tandawazi katika Kiswahili sanifu.

1.4 Maswali ya Utafiti

- i) Ni kipi chanzo cha lugha tandawazi.
- ii) Kuna athari gani zinazokiathiri Kiswahili sanifu kwa kutumia lugha tandawazi.

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utatoa mchango mkubwa baada ya kumalizika kwake hasa kwenye upande wa taaluma ya lugha na pia upande wa utamaduni. Kuna taasisi nyingi ambazo zitanufaika kwa kuutumia utafiti huu. Taasisi zenyewe kama Baraza la Kiswahili la Tanzania (BAKITA), Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) na watunga sera wa wizara ya elimu na mafunzo ya amali ya Zanzibar. Vilevile utafiti huu utakua ni marejeleo kwa wasomi wa lugha ya Kiswahili, pia wasomi na waandishi na watunzi wa vitabu vinavyohusu lugha tandawazi na wanafunzi wa ngazi mbali mbali za elimu.

Aidha, utafiti utatoa nafasi kwa wasomi na wtaalamu wengine kupata nafasi ya kupita kwa ajili ya kuzibapengo lililoachwa na mtafiti wa utafiti huu,na pia kutaua matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili yanayosababishwanahali tofauti kama vile vyombo vya habari, matumizi ya simu na mitandao mengine ya kijamii.

1.6 Hitimisho

Sura ya kwanza ambayo ni sura tangulizi imeeleza taaarifa zinahusiana na chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu. Sura imeanza kwa utangulizi, ambao umefuatiwa na usuli wa mada.Baada ya usuli wa mada mtafiti alibainisha tatizo la utafiti, akifatiwa na malengo pamoja na maswali ya utafiti. Aidha sura imezungumzia umuhimu wa utafiti pamoja na mipaka ya utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni kusoma maandiko na makala mbali mbali ambazo zina fupisha tafiti katika eneo fulani (Cozby, 2012). Mtafiti wa utafiti huu amesoma kazi ambazo zina- mahusiano na mada yake ya utafiti. Kazi ambazo zinazungumzia juu ya dhana ya chimbuko, dhana ya lugha, dhana ya utandaazi na pia zile zinazohusiana na usanfishaji. Mtafiti amezisoma kazi hizo kwa madhumuni ya kupata maarifa juu ya mada anayoitafiti na pia kubaini pengo la utafiti ambalo limeachwa na watafiti walio tangulia ili laweze kupunguza mwanya wa pengo hilo. Neno chimbuko lina maana ya mahali kitu au jambo lilipo anzia (Masamba, 1999).

2.2 Dhana ya Lugha

Kuna wataalamu mbalimbali ambao wamefasili maana ya lugha miongonimwao ni: (Nkwera 1979) ambae amesema kwamba lugha ni utaratibu au mfumo maalumu wa sauti za nasibu zenye maana ambazo hutumiwa miongoni mwa binaadamu kwa madhumuni ya mawasiliano miongoni mwao .na sauti hizo ni lazima ziwe za kutamkwa. TUKI (1981) wanasema wanaona kwamba lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana, mpangilio ambao hutumiwa na watu wa taifa au kabila fulani kwa ajili ya kuwasiliana. Kamusi ya Kiswahili (1990) inasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana.

2.3 Dhana ya chimbuko

Masamba na wenzake (1999) wanasema kwamba neno chimbuko lina maana ya mahali kitu au jambo lilipo anzia. Kamusi la Kiswahili fasaha (2010) chimbuko ni pahali jambo lilipo anzia na badae kuenea.

2.4 Dhana ya Utandawazi

Little (1996) ameeleza kwamba utandawazi ni fikra kwamba mipango yote ya kiuchumii, kisiasa na kiutamaduni inapaswa kuandaliwa kwa lengo la kuondoa mipaka ya taifa moja ili mipango kama hiyo iweze kutanda na hatimae kuenea dunia nzima. Nae Sweeting (1996) anasema kwamba utndawzi ni kuihusisha dunia ambayo ndio sayari mama na ni maskani yetu, maana yake ni kuiona dunia kama kitu kimoja na wtu wote ni wa kabila moja. Beekens (2006) anaona kwamba utandawzi ni utaratibu ambao watu katika dunia huunganishwa pamoja na kuwa kama kijiji. Katika mfumo wa utandawzi dunia huwa kama kijiji kimawasiliano kwani mawasiliano huwa rahisi.

2.5 Lugha Tandawazi

Kwa mujibu wa Mutembe (2011), lugha tandawazi ni lugha inayotumiwa mitandaoni wakati wa kuandika ujumbe, ni lugha ambayo hutumia mchanganyiko wa maneno wenye lugha zaidi ya moja na kuunda lugha nyengine tofauti. Aidha akasema lugha tandawzi ni lugha ya ufupisho, mara nyingi ufupisho huo hupatikana kwa njia ya kudondosha baadhi ya sauti na pia hupatikana kwa njia ya kuchanganya maneno pamoja na nambari. Mfano wa maneno yaliyo katika lugha tandawazi ni kama kusima100 = kusimamia, 208 = tuonane, cku2pi = siktupi.

Lugha tandawazi ni jambo ambalo liliwavutia wengi na wakaamua kulifanyia utafiti. Baadhi ya waliovutiwa na suala hilo ni kama: Mpahlela na Mashamaite (2005). Wawili hawa walichunguza kuhusu athari za ujumbe mfupi katika kupata umahiri wa lugha. Lengo la utafiti huo ni kufafanua namna ya lugha tandawazi inavyo athiri umahiri wa lugha kwa wanafunzi. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa lugha tandawazi haifuati sheria za kisarufi na haifuati kanuni za kitahajia. Watafiti hawa walitumia lugha ya Kiingereza na hawakuhusisha lugha nyengine.

Kingei na Kobia (2007) walichunguza kuhusu lugha ya sheng. Sheng ni lugha ambayo ina mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza. lengo la utafiti wao ni kufafanua asili na sababu ya kuzuka kwa lugha ya Sheng utafiti ulionesha kuwa ni ishara ya kuenea kwa lugha Sanifu ya Kiswahili na Kingereza. Watafiti waliangalia kuzuka kwa lugha ya Sheng na hawakuangalia athari zake katika lugha. Nao al-khatib na Sabah (2008) walichunguza lugha wakati wa uandishi wa ujumbe mfupi wa simu za kiganjani kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Jordan. Nia ni kuchunguza muundo waisimu jamii wa kubadili msimbo katika lugha ya Kiarabu na Kiingereza katika uandishi wa ujumbe mfupi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Jordan Morogoro.

Katika utafiti huu waligundua kuwa wanawake hupenda kutumia Kiarabu zaidi kuliko wanaume wakati wa uandishi wa ujumbe mfupi katika simu na wanaume hupenda kutumia lugha ya Kiingereza na pia kuchanganya lugha ya Kingereza na Kiarabu. Pia utafiti umeonesha sababu ya kubadli msimbo kuwa ni kurahisisha na kupata nafasi kwa kuandika lugha ya Kiarabu kuliko lugha ya Kiingereza.

Katika utafiti huu mtafiti alizingatia zaidi lugha inayotumika zaidi katika uandishi wa ujumbe mfupi katika simu za kiganjani na haukuzingatia muundo wa lugha unaotumika pamoja na athari zake.

2.6 Lugha ya Kiswahili na Usanifishaji

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo haitumiki Mfrika Mashariki tu bali hutumika katika Afrika ya Kati, Afrika ya Kusini na ulimwenguni kote. Lugha hii hufundishwa hata katika vyuo vikuu mbali mbali ulimwenguni kama vile Kenya, Tanzania na ulimwenguni kote (Habwe na Karanja 2004).

2.7 Kiswahili Sanifu

Kiswahili Sanifu ni lahaja inayotokana na Kiunguja mjini lahaja ambayo imekubaliwa kuwa itumike kwa jamii ya wazungumzaji kuwa ni kioo cha ufasaha katika jamii nzima ya Waswahili wa eneo la upwa wa Afrika Mashariki na visiwa vyake. (Makame (2007). Maandiko ya zamani ya kazi ya Kiswahili ni yale maandiko ya Stere (1970) ambayo yalizungmzia usanifishaji wa KiswahiliKrap na Stere (1930-1931) waliksanifisha Kiunguja mjini na kuwa ndio lahaja ya Kiswahili Sanifu.

Mbaabu (1991) alieleza kuwa kulikuwa na lahaja nyingi katika Afrika Mashariki lakini hata hivyo lahaja ya Kimvita na lahaja ya Kiunguja mjini zilikuwa na ushindani mkubwa katika kuteua lahaja itakayofaa kuwa lahaja ya msingi kutumika katika Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kiunguja mjini ndio lahaja iliyoteuliwa kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu. Na kazi hii ilipelekea kurahisisha kujua historia ya lugha ya Kiswahili na Usanifishaji wake. Nae Dadi (1995) ameelezea juu ya matumizi mabaya ya lugha katika vyombo vya habari .ambapo amegusia kuhusu

mchakato wa vyombo vya habari katika matumizi ya misamiati mipya. Idarus (2005) yeye ameelezea juu ya matumizi mabaya ya Kiswahili kwa watumiaji wa vyombo vya habari nae pia ametaja makosa ya kimsamiati, miundo ya sentensi na matamshi kwa watendaji wa vyombo vya habari. Pia Makame amechunguza juu ya matumizi ya Kiswahili Sanifu kwa watangazaji wa sauti ya Tanzania Zanzibar.

2.8 Pengo la Utafiti

Mtafiti wa utafiti huu alisoma kazi mbalimbali ambazo zilitangulia hapo awli na akabaini ya kwamba dhana ya lugha tandawazi ni maarufu sana. Dhana hii imediriki kufanyiwa utafiti na watafiti wengi ulimwenguni, lakini alichogundua matafiti ni kwamba kazi zote hizo za utafiti dhana ya chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu haijawahi kufanyiwa utafiti na ndio maana mtafiti wa utafiti huu akaamua kuifanyia utafiti mada hii ili kupunguza mwanya ulioachwa na watangulizi wake.

2.9 Kiunzi cha Nadharia

2.9.1 Maana ya Nadharia

Masamba na wenzake (2009) wanasema kuwa nadharia ni utaratibu, kanuni au misingi iliojengwa kimawazo kwa madhumuni ya kuwa kigezo cha kueleza jambo au mambo kadhaa. Mdee na wenzake (2011) wansema nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani.

Nadharia ni mawazo yanayotumika kuwa muongozo wa kutekeleza jambo au kutambulika kwa dhana (BAKIZA 20010). Kwa hiyo na dharia ni mpangilio na utaratibu maalumu wakuelekeza na kufahamisha jinsi ya utendaji wa mambo fulani

fulani. Mtafiti wa utafiti huu alitumia nadharia kidhi katika utafiti wake kwa kuamini kwamba ndiyo itakayo muelekeza kufikia malengo yake.

Nadharia kidhi ya mawasiliano (NKM) imeanzishwa mwaka (1973) na muasisi wake ni Giles kwa lengo la kueleza sababu za kubadili mtindo wa matamshi wakati wa kuwasiliana na athari zake katika jamii. Nadharia kidhi (NKM) inaamini kwamba binaadamu hujitahidi kuzungumza lugha au kuiga namna ya matamshi ya lugha ya msikilizaji wake ilil aweze kutimiza haja ya mawasiliano kwa kujua au kutojua na kwa makusudi au kwa bahati mbaya .Binaadamu huiga msamiati au vipengele vyengine vya lugha kwa mtu anaezungumza nae. Pia mawasiliano ya kiisimu hufasiliwa kama mbinu, kwa sababu watu huiga mawasiliano yanayotumiwa na watu wengine kwa lengo la kukubalika katika jamii.

Sababu ya kubadili mtindo wa matamshi ni kuonesha makubaliano na mahusiano kwa watu wengine na kitendo hiki huwafanya watu wajihisi kuwa ni wa moja. Mawasiliano katika nadharia kidhi yamejigawa katika makundi mawili ambayo ni mawasiliano wima na mawasiliano yasio wima. Mawasiliano wima ni yale mawasiliano ambayo hutokea pale ambapo mtu anapozungumza na mtambuzi wa lugha hujilazimisha kuzungumza lugha yake.

Mawasiliano yasio wima ni mawasiliano ambayo hutokea pale ambapo mtu anapozungumza hurahisisha lugha ili kukidhi haja ya mawasiliano. Nadharia kidhi (NKM) inaamini: Mawasiliano huathiriwa kutokana na watu wanavyopokea pamoja na kutathmini nini kimetokea katika mazungumzo (namna watu wanavyotafsiri

ujumbe ulio badilishwa katika mazungumzo. Mawasiliano hubadilika kutokana na kanuni pamoja na hali ya muktadha inaofaa.

Watu hueleza historia na uzoefu wao katika mawasiliano kwa kupitia matamshi na tabia zao kwa kuonesha kuwepo ufanano wa matamshi na tabia fulani katika mazungumzo. Sababu za kutumia nadharia kidhi (N.K.M.) ni kama zifuatazo: Nadharia kidhi inazungumzia habari za mawasiliano, ambapo na utafiti huu nao unazungumzia mawasiliano vilevile. N.K.M. pia inazungumzia sababu za kubadili mtindo katika matamshi na utafiti huu nao unazungumzia chimbuko lugha tandawazi katika Kiswahili sanifu. N.K.M. Ilimsaidia mtafiti wa utafiti huu kujuwa kuwa watu wanapowasiliana hutumia lugha iwe kwa ukamilifu wake au kwa kupunguza baadhi ya sauti na hata kuchanganya lugha au kuchanganya maneno na nambari.

2.10 Hitimisho

Katika sura ya pili mtafiti alizungumzia kuhusiana na mapitio ya kazi tangulizi, kiunzi cha nadharia na kubainisha pengo la utafiti. Kwa jumla imebainika kuwa bado hakujafanyika utafiti wa kutosha katika eneo hili tulilolichagua na hivyo tumeona kuwa ipo haja ya kufanya utafiti huu ili kukuza maarifa na kujaza pengo la utafiti.

SURA YA TATU

NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imewekwa ili kufafanua namna ya utafiti ulivyofanyika. Sura hii inaeleza kwa uwazi eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji. Sura hii pia inafafanua kwa kina mbinu za kukusanyia data na kuainisha vifaa vilivyotumika katika utafiti huu pamoja na hitimisho. Katika sura hii pia mtafiti ameelezea utaratibu wa utafiti aliotumia katika kuzichambua data hizo na kuzitolea taarifa zake.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar, ndani ya kisiwa cha Unguja katika mkoa wa mjini magharibi. Mtafiti amechagua eneo hili kwa sababu katika mkoa wa mjini magharibi ndipo mtafiti alipopata wilaya yenye msingi wa Kiswahili Sanifu na pia matumizi ya lugha tandawazi yanafanyika katika mkoa huo kuliko maeneo mengine ya hapa Unguja. Mkoa wa mjini magharibi ni mkoa ulioko magharibi ya Kisiwa cha Unguja ambao una jumla ya wilaya tatu ambazo ni wilaya ya mjini, wilaya ya magharibi A na wilaya ya magharibi B.

3.3 Sampuli na Usampulihaji

Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli ni kundi dogo la watafitiwa ambalo huchaguliwa kutoka kundi kubwa ili mtafiti kupata data na kutoa mahitimisho yake. Babbie (1992) anasema kuwa sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambao mtafiti anavutiwa nayo kwa kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Mtafiti wa utafiti huu alichagua sampuli lengwa (kukusudia) kulingana na sifa na uwezo wa

kutoa data sahihi kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu na pia sifa ya kuweza kutoa jibu sahihi kwa mujibu ya walivyoulizwa na mtafiti.

3.4 Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi legwa (sigh 2007). Kothari (2004) usampulishaji ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za uteuzi kwa washiriki kutoka kwenye kundi kubwa la watafitiwa. Fasili hii ina maana kuwa usampulishaji ni mbinu ya kuchagua ambapo sehemu ya watafitiwa huchaguliwa kwa kuzingatiwa upatikanaji wao na hauzingatii uwakilishi wao. Sampuli ya kukusudia ni sampuli ilyo chaguliwa na mtafiti kwa makusudi kwa kujua kwamba mtafitiwa fulani ndie ataetoa majibu sahihi ya utafiti. Sampuli ya kukusudia, sampuli ambayo ndio ilyo tumika katika utafiti huu.

3.5 Watafitiwa/Kundi lengwa

Watafitiwa ni sehemu ya jamii ya watu au vitu fulani vilivyochaguliwa ili kutoa taarifa zinazowakilisha jamii nzima (Kothari 2009:55-56). Watafitiwa katika utafiti huu ili wapatikane mtafiti alitumia mbinu ya kukusudia kwa kupata data zinazohitajika. Watafitiwa wote waliteuliwa wa kutumia mbinu ya kukusudia ambayo imeasisiwa na kothari (2008).

Walliman (2001) ameeleza kwamba kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti. vitu vilivyokusudiwa hapa ni kama vile watu, taasisi au matukio. Katika utafiti huu watafitiwa\kundi lengwa ni: wataalamu wa lugha ya Kiswahili, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), walimu wa skuli ya

fuoni sekondari, watoto wa miaka 12-18 katika mtaa wa fuoni kibonde mzungu, Vijana (wanafunzi) wa kidato cha sita katika shule ya sekondari ya hamamni na wazee wa mtaa wa Darajani.

Mtafiti aliamua kuchagua walengwa hao kwani ndio anaohisi wana uwezo wa kutoa taarifa zilizo sahihi ambazo zinahitajika katika utafiti huu. Kothari (keshatajwa) anasisitiza kwamba katika uteuzi wa sampuli usiwe mkubwa wala mdogo bali uwe wa kati na kati. Mtafiti wa utafiti huu amelizingatia hilo na yeye ameamua kuteua walengwa 80, kati ya hao wanawake 40 na wanaume 40.

Jedwali 3.1: Jedwali la Mchanganuo wa Watafitiwa / Kundi Lengwa

Wahusika	wanawake	Wanaume	Jumla
Wataalamu Wa lugha	15	15	30
Wafanya kazi	10	10	20
Watoto Miaka 12-18	05	05	10
Vijana	05	05	10
Wazee	05	05	10

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

Kutofautiana kwa idadi ya watafitiwa kumesababishwa na malengo ya utafiti, mtafiti alilenga zaidi kwa wataalamu wa lugha na wafanya kazi ambao mtafiti ana hisi ndio wataotoa data nyingi katika utafiti huu. Ambao ndio hasa watumiaji wa lugha tandawazi.

3.6 Mbinu za Utafiti

Mbinu za kukusanyia data ni mbinu zote zinazotumiwa kwenye utafiti. Mbinu hizo zimegawika katika makundi mawili ambayo ni mbinu ya kukusanyia data na mbinu ya kuchanganua data. Mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti wake. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya hojaji, mahojiano na mbinu ya ushuhudiaji.

3.6.1 Mbinu ya Ushuhudiaji

Ni mbinu inayohusu kusoma na kuchunguza tabia za watu, vitu na matukio kwenye mpangilio maalumu. Katika mbinu hii mtafiti huweza kupata taarifa za awali ambazo ndizo taarifa za msingi katika utafiti. Aidha mbinu hii husaidia kupunguza mapungufu yatakayoweza kujitokeza kwenye utafiti. Data za awali ni zile data za kuaminika kwa sababu data hizo zimepatikana kutoka kwenye tukio moja kwa moja.

3.6.2 Mbinu ya Mahojiano

Mosha (2004: 77) anasema kwamba, mbinu ya mahojiano ina faida nyingi, miongoni mwa faida hizo ni kwamba mbinu hii ni yenye kutumia muda mchache. Kombo na Tromp (2006) wao wanaelezea kwamba mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana kati ya watu wawili au zaidi kwa minajili ya kukusanya taarifa au maoni kuhusu jambo Fulani la kiutfiti lililo ainishwa. Kwa mujibu wa Walliman (2011) mahojiano yamegawika katika sehemu tatu ambazo ni mahojiano ya ana kwa ana, mahojiano ya kikundi na mahojiano ya simu (mitandao). Mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti hutoa fursa ya kuwauliza maswali watafitiwa na watafitiwa nao huweza kumuliza maswali mtafiti Kothari (2009).

Mtafiti wa utafiti huu aliamua kutumia mbinu hii kwaVijana na wazee sababu zifuatazo: Sababu ya kwanza ni mbinu ambayo taarifa zake huwa na ukweli kwa kiasi kikubwa. Pili, kwa kutumia mbinu hii mtafiti huweza kuidhibiti sampuli yake kwa kiasi kikubwa mno. Na sababu ya tatu mtafiti huweza kukusanya taarifa nyingi zaidi kwa muda mfupi.

3.6.3 Mbinu ya Hojaji

Kothari (keshatajwa) anasema kuwa hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti huandika maswali, na kisha maswali hayo hupewa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti. Wamitilia (2003:62) anaeleza kuwa hojaji ni mbinu inayotumiwa kuelezea maswali anayoyatumia mtafiti kama ni msingi wa utafiti wake. Mugende (2003) anasema kuwa hojaji huandaliwa ili kukusanya taarifa muhimu kutoka kwa watafitiwa.

Walliman (keshatajwa) yeye ameyagawa maswali ya hojaji katika makundi mawili, ambayo ni maswali funge na maswali yasiokuwa funge. Maswali funge ni yale maswali ambayo hutoa tarifa kwa watafitiwa kuchagua jibu. .Aina hii ya maswali huwa rahisi kujibu na inamsaidia mtafiti kupata majibu mahsusi na pia kuepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ni maswali yasio funge. Maswali yasiyo funge hutoa fursa kwa watafitiwa kuwa huru ili kueleza wanachokijua. Aina hii ya maswali hutoa uhuru kwa watafitiwa kueleza mawazo yao na mtafiti huweza kupata taarifa nyingi zaidi.

Katika utafiti huu mtafiti alitumia aina zote mbili za maswali ili kuepuka mapungufu na makosa kwa sababu kila aina moja ya maswali inayomapungufu yake. Watafitiwa ambao ni wataalamu wa lugha na wafanyakazi, walipewa hojaji wazijaze na baada ya

siku tano mtafiti alizifuata kwa ajili ya kuzikusanya na kuzifanyia uchambuzi. Watafitiwa hawa wamepewa muda kutokana na majukumu yao kikazi mtafiti alidhani kuwa ni vigumu kupata data za papo kwa papo. Kwa upande wa watoto, vijana na wazee wao walipewa hojaji na walizijaza papo kwa papo. Mtafiti aliamua kutumia mbinu ya hojaji kwa sababu kwenye kundi kubwa la watu ndio mbinu yenye kufaa zaidi na ni rahisi na haraka katika ukusanyaji wa data.

3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupanga vizuri taarifa zilizokusanywa kwa lengo la kukamilisha malengo ya utafiti (Babbie 1999). Kwa mujibu wa Kothar (keshatajwa) amesema uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika utafiti ambapo humsaidia mtafiti kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Katika utafiti data huchambuliwa kupita mikabala ya aina mbili ambayo ni mikabala ya kiidadi na mikabala isio ya kiidadi. Mkabala wa kiidadi Walliman ambae (keshatajwa) anaeleza kuwa ni mbinu ya kuchambua data kwa kutumia tarakimu (nambari). Nae Kothari (keshatajwa) anasema mkabala wa kiidadi ni mbinu ya uchambuzi wa kitakwimu. Hii ni mbinu inayo husisha tarakimu kama vile asilimia kutokana na idadi ya watafitiwa.

Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Pia Kress (2008) amesema kwamba mkabala usio wa kiidadi hueleza vipi au kwa nini tukio limetokea. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mkabala wa kidadi na mkabala usio wa kiidadi kwa kujua kwamba kila mkabala una umuhimu wake katika utafiti.

3.8 Hitimisho

Katika sura ya tatu ambayo ni njia na mbinu za utafiti sura hii imezungumzia eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, watafitiwa, vifaa vya kukusanyia data, mbinu za kukusanyia data pamoja na mbinu za kuchanganua data. Sura inayofuata inahusiana na uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data za mada ya utafiti yenye kichwa cha habari Chimbuko la Lugha Tandawazi na Athari zake katika Kiswahili Sanifu. Data zinazowasilishwa na kuchambuliwa, ni zile ambazo zimekusanywa kwa kutumia mbinu mbali mbali. Miongoni mwa mbinu hizo ni hojaji, mahojiano na uchunguuzi. Data hizi zinawasilishwa na kuchambuliwa kwa kufafanuliwa kwa uwazi zaidi ndani ya sura hii.

Katika utafiti huu mtafiti ametumia data za msingi, ambazo zimekusanywa na mtafiti kutoka uwandani. Mtafiti wa Utafiti huu amekusanya data na amezigawa katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusiana na data zinazohusu chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu na kundi la pili linahusudata zinazohusiana na athari ya lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu.

Mtafiti ameamua kuigawa sampuli yake katika makundi matano ili iwerahisi kwake katika kulinganisha matokeo ya watafitiwa wake. Sura ya nne inaanza kwa uwasilishaji wa data na itamalizia kwa uchambuzi na ufafanuzi pamoja na uchanganuzi wa data kama ifuatavyo:

4.2 Chimbuko la Lugha Tandawazi katika Lugha Sanifu

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha chimbuko la lugha tandawazi katika Kiswahili sanifu. Mtafiti baada ya kukusanya taarifa kutoka kwa

watafitiwa kwa kutumia mbinu za utafiti ambazo ni mbinu ya mahojiano, mbinu ya hojaji, mbinu ya uchunguzi na baada ya kupata majibu ya maswali kutoka katika makundi matano aliwasilisha data yake kama ifuatavyo:-

Jedwali na 4.1 : Majibu ya Watafitiwa

	Wazungumzaji wa lugha	Watumiaji wa Simu	Taasisi za Kielimu
Sampuli A	19	08	03
Sampuli B	12	06	02
Sampuli C	05	04	01
Sampuli D	06	04	00
Sampuli E	10	00	00

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

Katika utafiti huu, watafitiwa walijaza dodoso na walishiriki kujibu maswali kwa kutumia mbinu ya mahojiano. sampuli A walishiriki watafitiwa 30 ambapo watafitiwa kumi na tisa (19) kati yao walisema chanzo cha lugha tandawazi wazungumzaji wa lugha, watafitiwa 08 wamesema chimbuko la lugha tandawazi ni watumiaji wa simu na watafitiwa 3 wao wamesema kua chimbuko la lugha tandawazi ni taasisi za kielimu. Sampuli B watafitiwa 12 wamesema chimbuko la lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha ,watafitiwa 6 wamesema chimbuko la lugha tandawazi ni watumiaji wa simu na watafitiwa 3 wamesema Chimbuko la lugha tandawazi ni taasisi za kielimu.

Watafitiwa wa sampuli C walikuwa 10 ambapo watafitiwa watano (05) walisema Chimbuko cha lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha. Watafitiwa wanne (4) wamesema chimbuko la lugha tandawazi ni watumiaji wa simu na mtafitiwa mmoja (1) amesema kuwa chanzo cha lugha tandawazi ni taasisi za kielimu. Sampuli D watafitiwa nao walikuwa kumi (10) ambapo sita (6) kati yao wamesema wazungumzaji wa lugha ndio chanzo cha lugha tandawazi na watafitiwa wanne (4) wamesema kuwa chanzo cha lugha tandawazi ni watumiaji wa simu. Sampuli E ilikuwa na watafitiwa kumi (10), ambapo wote walidai kwamba chanzo cha kutumika lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu ni wazungumzaji wa lugha.

4.2.1 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Chimbuko la Lugha Tandawazi

Utafiti huu ulikuwa na jumla ya watafitiwa themanini (80). Watafitiwa hao waligawanywa katika sampuli tano (5) ambazo ni sampuli A, sampuli B, na sampuli C. Vilevile utafiti ulikuwa na sampuli D pamoja na sampuli E. Katika sampuli A, kulikuwa na watafitiwa 30 ambao walijibu swali lililoshikamana na lengo kuu la utafiti huu ambalo lilimtaka mtafiti athibitishe iwapo chimbuko la lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha wenyewe au la. Waliokubali kuwa chimbuko la lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha walikuwa ni watafitiwa 19 kati ya watafitiwa 30 sawa na asilimia sitini na tatu nukta tatu (63.3%). Katika sampuli B watafitiwa kumi na mbili 12 kati ya ishirini sawa na asilimia sitini (60%) walikiri kwamba wazungumzaji wa lugha ndio chanzo cha lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu. Pia katika sampuli C watafitiwa 05 kati ya kumi sawa na asilimia hamsini (50%) nao walisema kuwa lugha tandawazi chimbuko lake ni wazungumzaji wenyewe wa Lugha. Vile vile sampuli D yenye watafitiwa kumi (10) sita (06) kati yao sawa na

asilimia (60%) walisema kuwa wazungumzaji wa lugha ndio chimbuko la lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu. Pia katika sampuli E watafitiwa wote kumi (10), sawa na asilimia mia (100%) walikiri kwamba wazungumzaji wa lugha ndio chanzo cha lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu.

Kutokana na matokeo haya mtafiti anakubaliana na watafitiwa ambao wamechukua asilimia kubwa kwa kusema kuwa chanzo cha lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha na sio watumiaji wa simu au taasisi za kielimu.

Jedwali na: 4.2 Jinsia za Watafitiwa

	Wanawake	Wanaume	Jumla
Sampuli A	15	15	30
Sampuli B	10	10	20
Sampuli C	05	05	10
sampuliD	05	05	10
Sampuli E	05	05	10
Jumla kuu	40	40	80

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

Ufunguo:

Sampuli A = Wataalamu wa Lugha.

Sampuli B = Walimu

Sampuli C = Watoto wa Miaka 12 -18

Sampuli D = Vijana wa Miaka 18 -40

Sampuli E = Wazee

Kwa upande wa jinsia, wazungumzaji wengi wa lugha ambao ndio chimbuko la lugha tandawazi ni wanawake, hii ni kutokana na kwamba wanawake wengi waliotafitiwa wamesema chimbuko la lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha wenyewe. Katika sampuli A wanawake 15 wamekiri kuwa lugha tandawazi imeanzishwa na wazungumzaji wa Lugha. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na kile cha wanaume wanne tu walioikiri hali hiyo. Katika sampuli B watafitiwa wanawake wanane (08) wamesema lugha tandawazi chimbuko lake ni wazungumzaji wa lugha wenyewe. Kiwango hiki pia ni kikubwa ukilinganisha na kile cha wanaume wanne tu waliolikubali shauri hilo. Kwenye sampuli C wanawake wanne (04) wamekiri kwamba wazungumzaji wa lugha ndio chimbuko la lugha tandawazi. Kiwango hiki pia ni kikubwa ukilinganisha na mtafitiwa mmoja tu mwanamme aliyekubali wazo hili. Katika sampuli D wanawake watano (5) wamesema kuwa chanzo cha lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na cha mwanamme mmoja tu aliyekiri jambo hili. Katika sampuli E watafitiwa wote watano (05) wanawake wamesema kuwa wazungumzaji wa lugha ndio chimbuko la lugha tandawazi.

Kwa matokeo haya ni dhahiri kuwa wanawake wanachangia asilimia kubwa katika kuibua lugha tandawazi kwenye mazungumzo yao. Hii ina maana kwamba wanawake wengi ama huchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja au huchanganya maneno na herufi katika maandishi yao ya ujumbe.

Ingawaje wanawake wanaongoza katika kutumia lugha tandawazi na wanaume nao pia wamekubali kwamba lugha tandawazi chimbuko lake ni wazungumzaji wa lugha. Katika sampuli A watafitiwa wanne (4) wanaume wamesema kuwa wazungumzaji

wa lugha ndio chanzo cha lugha tandawazi. Katika sampuli B watafitiwa wanne (04) nao wamekubali ya kuwa wazungumzaji wa lugha ndio chimbuko la lugha tandawazi. Katika sampuli E idadi ya watafitiwa iko sawa baina ya wanawake na wanaume. Maelezo haya yanatoa msisitizo ya kwamba wazungumzaji wa lugha ndio chanzo cha kuibua lugha tandawazi katika jamii.

4.3 Uchanganyaji wa Lugha Mbili wakati wa Mawasiliano

Mtafiti amebaini kwamba waongejaji wengi aliohojiana nao hupenda kutumia lugha tandawazi kama alivyofafanua katika kipengele 4.2.1 hapo juu. Matumizi ya lugha kama hiyo yameainishwa katika jedwali nambari 4.3 hapo chini:-

Jedwali na: 4.3 Mifano ya Sentensi zilizochanganywa Lugha Mbili kwa Wakati Mmoja

Sentensi	Neno lililo changanywa	Maana ya Sentensi
Utaniwait kidogo	Wait	utaniubiri kidogo
Baadae ni call	Call	baadae ni pigie
Nina problem	Problem	nina tatizo
Njoo just ni kuone	Just	njoo japo nikuone
Mpe mzigo anco wako	Anco	mpe mzigo mjomba wako
Ok baadae	Ok	haya baadae
Face yake ya ucheshi	Face	uura yake ya ucheshi

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

4.3.1 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Uchanganyaji wa Lugha Mbili wakati wa Mawasiliano

Watafitiwa walio wengi wamekubali kuwa lugha tandawazi imeibuliwa na wazungumzaji wa lugha kutokana na mazungumzo yao. Waongeaji wa aina hii huwa hawazingatii matumizi ya lugha Sanifu na ndio hapo huzaliwa lugha tandawazi. Lugha tandawazi huwekwa katika sura mbili ambazo ni kuchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja na kucha nganya herufi na nambari hasa wakati wa kutumiana ujumbe iwe kwa njia ya simu au kwa njia ya barua pepe au kwa maandishi ya aina yoyote.

Wazungumzaji wa lugha waliowengi huchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja. Mfano huchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza au huchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiaraabu. Wazungumzaji wote hawa hutumia lugha hizi kwa malengo ya kupata mawasiliano katika mazungumzo yao. Katika sampuli A miongoni mwa watafitiwa 19 ambao walisema kuwa chimbuko la lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha, watafitiwa 17 walionekana kuwa wanachanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza na watafitiwa 02 huchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu. Katika sampuli B watafitiwa 12 huchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Katika sampuli C, watafitiwa 05 katika mazungumzo yao huchanganya lugha mbili wakati wanapo zungumza, na katika sampuli D watafitiwa 10 hutumia lugha tandawazi katika mawasiliano yao na wengi wao huchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja ambayo ni lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza katika mawasiliano yao. Katika sampuli E watafitiwa 10 wamekiri kuwa wazungumzaji wa lugha ndio chanzo cha lugha tandawazi lakini wao hawatumii lugha tandawazi katika mawasiliano yao.

4.3.2 Lugha zilizochanganywa katika sampuli A

Sampuli A ndiyo iliyoongoza kwa watafitiwa wengi waliokiri kwamba wazungumzaji wa lugha ndiyo chanzo kilicholeta lugha tandawazi. Waongejaji wa lugha ya aina huyo hujikuta wanaongea lugha mchanganyiko inayochanganya baina ya Kiswahili na Kiingereza, baina ya Kiswahili na Kiarabu na baina ya Kiswahili na nambari.

4.3.2.1 Mchanganyiko kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza

Waongejaji wengi wa lugha tandawazi hujikuta wanachanganya lugha wakati wa mazungumzo. Hujikuta ingawa wanazungumza Kiswahili lakini lugha yao imesheheni tele maneno ya Kiingereza.

Jedwali na.4.4 :Mchanganyiko wa Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kiingereza

Seentensi	Maana ya Sentensi / Neno
Nakutakia good night	nakutakia usiku mwema
Bye	kwaheri
Tutaonana tomorrow	uutaonana kesho
Ni beep	Nishitue

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

4.3.2.2 Mchanganyiko kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiarabu

Wapo baadhi ya waongejaji wa lugha wanaotumia lugha tandawazi, wapendao kutumia lugha ya Kiswahili kilichochanganyika kwa kiasi kidogo cha Kiarabu. Hata hivyo idadi hii kwa mujibu wa data tulizonazo sio kubwa hata kidogo. Mifano yake imeoneshwa hapo juu kama ifuatavyo:-

Jedwali nambari: 4:5 Mchanganyiko wa Lugha ya Kiswahili na Lugha ya

Kiarabu

Sentensi	Neno la Kiarabu	Maana ya sentensi
Nakwenda madrasa	Madrasa	nakwenda skuli
Nimeswali katika masjid	Masjid	nimeswali msikitini
Hayaat Karume	Hayaat	marehemu Karume
Lete kayfa	Kayfa	lete habari
Natoka bayt	Bayt	natoka nyumbani

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

4.3.2.3 Mchanganyiko wa Maneno na Nambari katika Uandishi

Watumiaji wa lugha tandawazi katika kuandika mara nyingi hutumia nambari na lugha katika uwasilishaji wa nyijumbe/jumbe za simu za mkononi. Jedwali nambari 4.6 linahusika na uwasilisha wa data alizoashiria mtafiti hapo juu:

Jedwali na.4.6: Mifano ya Sentensi zilizo changanywa Maneno na Nambari

Sentensi	Nambari iliyo changanywa	Maana ya Sentensi
2mekuja kwa 7bu yako	2na 7	tumekuja kwa sababu yako
2po pamoja	2	tupo pamoja
Jioni muo8	8	jioni muonane
Watu wote wameu100	100	watu wote wameumia
6taki kuchezewa	6	sitaki kuchezewa
4rodhani ndio nyumbani	4	forodhani ndio nyumbani
Wanangu nawasima100 kazi zao	100	wanangu nawasimamia kazi zao

Chanzo kutoka Uwandani (2018)

4.3.3 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Mchanganyiko wa Maneno na Nambari katika Uandishi

Wazungumzaji wengi wa lugha hutumia mtindo huu wa kuchanganya lugha. Mchanganyiko huu mara nyingi unakuwa kati ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu au lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza na hata kuchanganya maneno na nambari katika mawasiliano yao. Katika mawasiliano hayo wazungumzaji walio wengi huchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza kutokana na kuwa Kiingereza ni lugha inayopendwa na vijana walio wengi na kudhaniwa kuwa ni lugha ya kileo au ni lugha yenye ustaarabu yenye hadhi kubwa kwao. Kiingereza ni lugha ambayo katika nchi ya Tanzania inatumika kama lugha rasmi na lugha ya pili itumikayo kwa ajili ya mawasiliano na kama lugha ya kufundishia kwenye taasisi za elimu ya juu. Kwa mfano katika kisiwa chetu cha Zanzibar Kiingereza katika skuli za msingi ni somo maalum linalofundishwa, katika skuli za sekondari Kiingereza ni lugha ya kufundishia na katika vyuo vikuu pia kiingereza ni lugha ya kufundishia. Kwa hiyo vijana walio wengi huathiriwa na Kiingereza katika mazungumzo yao.

Lugha ya Kiarabu ni somo linalosomeshwa katika ngazi zote za kielimu Hata hivyo watu waliowengi huwa hawakipendi Kiarabu na kuona kuwa ni lugha iliyopitwa na wakati. Kutokana na sabaabu hizi ndio maana wazungumzaji walio wengi hutumia Kiswahili na Kiingereza katika mazungumzo yao na wanapowasiliana kwa njia ya simu hutumia nambari ambazo hutamkwa kwa Kiingereza kuwakilisha neno la Kiswahili.

**Jedwali na. 4.7: Mifano ya Lugha Tandawazi wanayotumia Wazungumzaji wa
Lugha katika Mazungumzo yao au kwa Njia ya Ujumbe katika
Mawasiliano yao**

Lugha Tandawazi	Neno /Maneno ya Kiutandawazi yaliyoingizwa	Ufafanuzi kwa Lugha Sanifu
Niko alone	Alone	niko peke yangu
Baadae nicall	Call	baadae nipigie simu
Yuko kwenye bad	bad	yuko kitandanic(amelala)
Hujambo you	You	hujambo wewe
Nakwenda home kusleep	home na sleep	nakwenda nyumbani kulala
Anco wako atakubeep baadae	anco na beep	mjomba atakushtua kwa simu baadae
Kufahamu ni easy tu	Easy	kufahamu ni rahisi
Anatoka masjid kupray	Masjid na kupray	anatoka mskitini kuswali
Hayaat mzee karume ni rais wa kwanza wa Zanzibar	Hayaat	marehemu mzee Karume ni rais wa kwanza wa Zanzibar
2natoka madrasa	2 na madrasa	Tunatoka skuli
Vp leo utakuja ?	Vp	Vipi leo utakuja
Ni2mie sms	2 na sms	Nitumie ujumbe
Cm yake imepotea	Cm	Simuyake imepote
Good 9t	Good na9	Usiku mwema
Alinifollow kwa 7bu anashida na mie	Follow na 7	Alinifuata kwasababu anashida na mie
juma ameanguka na amezi100	100	Juma ameanguka na amezimia

J5 kk amewasili nchini	Kk na j5	Jumaatano Kaka amewasili nchini
Alinitumia habari ya mku5 siku ya j2	5 na j2	Alinitumia habari ya mkutano jumaapili
Haraka zako zili7bisha mttz mng	7 na mttz na mng	Haraka zako zilisababisha matatizo mengi
Hjmb,mm na kucalimia	Hjmb , mm na kucalimia	Hujambo mimi na kusalimia
Sw 2onane morrow	Sw , 2 na marrow	Sawa ,tuonane kesho
Ktk haya hamna problem	Ktk na problem	Katika haya hakuna matatizo
Bc 6ki kwenda tena 4ro	Bc , 6na 4	Basi sitaki kwenda tena forodhani.
Sn shida nw mm nimstaarabu 2	Sn ,nw , mm na 2	Sina shida na wewe mimi ni mstaarabu tu
Co lazima 2weke mku5 leo	Co , 2 na 5	Sio lazima tuweke mkutano leo
Baadae 2o8 home	2o8 na home	Baadae tuonane nyumbani
M2 wangu ameu100 mguu	M2 na 100	Mtu wangu ameumia mguu
Fa2ma anaishi saa10	2 na 10	Fatuma anaishi saateni
Wajiriwa wamejaza 4mu za mkataba wa kz	4 na kz	Wajiriwa wamejaza fomu za mkataba wa kazi
7bu kubwa ya kufungwa skuli ni mvua	7	Sabu kubwa ya kufungwa skuli ni mvua
2mepoteza md kwa 7bu 2nataka 2o8 naww	2 , md , 7, na 2o8	Tumepoteza muda kwa sababu tunataka tuonane na wewe

Chanzo: Data kutoka Utafiti huu (2018)

4.3.4 Tafsiri ya Matokeo Matumizi ya Lugha Tandawazi kwenye Ujumbe wa Maandishikwa njia ya wasap kupitia Simu za mkononi

Lugha tandawzi hutumika sana katika jamii, waandishi wa lugha hutumia maneno mengi yenye sura ya lugha tandawazi na mara nyingi watumiaji hao hutumia maneno yenye sura ya lugha tandawazi hasa hutumia mchanganyiko kati ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kuliko vile wanavyochanganya Kiswahili na Kiarabu lugha ya kiarabu. Watafitwa walio wengi hutumia mchanganyiko lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwenye mazungumzo yao na hata kwenye mawasiliano yao kwa njia ya simu. Watafitiwa wa utafiti huu wamesema sababu ya kutumia lugha ya Kiingereza katika mawasiliano kwa sababu Kiingereza ni lugha iliyoenea na pia inatambulikana na watu wengi ukilinganisha na lugha ya Kiarabu.

Jedwali Na 4.8: Idadi ya watafitiwa wanaotumia Lugha ya Kiingereza na Kiswahili na wanao tumia Lugha ya Kiarabu na Kiswahili

Sampuli	Kingereza na kiswahili	Kiarabu na kiswahili	Jumla
Sampuli A	20	5	25
Sampuli B	9	5	14
Sampuli C	5	1	06
Sampuli D	9	-	09
Sampuli E	-	3	03
Jumla	43	13	57

Chanzo kutoka katika utafiti huu (2018)

Lugha tandawazi hutumika katika kiwango cha neno na kiwango cha sentensi. Katika kiwango cha neno mzungumzaji huchanganya lugha mbili katika mazungumzo yake. Kwenye sentensi ambayo inayo maneno sita, au matano na hata manne baaandi ya neno hulipa sura ya lugha tandawazi.

Jedwali na. 4.9: Lugha Tandawazi katika Kiwango cha Maneno

Neno lenye Sura ya Lugha Tandawazi	Maana ya neno
Nyngn	Nyengine
Kk	Kaka
6ki	Sitaki
7bu	Sababu
M2	Mtu
2o8	Tuonane
Fa2ma	Fatuma
Lkn	Lakini
Co	Sio
Saa10	Saateni
Kuzi100	Kuzimia

Chanzo kutoka utafiti huu (2018)

4.3.5 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Lugha Tandawazi kwenye Kiwango cha Maneno

Kutokana na maneno haya wazungumzaji wa lugha katika kuwasiliana kwao wametumia kanuni ya udondoshaji, na mtindo huu wa lugha tandawazi hutumika

hasa wakati wa kuandikiana ujumbe kwa njia ya simu. wazungumzaji hao wamedondosha irabu zote katika maneno waliyo ya fupisha. Mfano neno lkn, nyngn, vp, hjmb, mzm na maneno mengineyo. Pia wazungumzaji wametumia mtindo wa lugha tandawazi wa kuchanganya nambari na maneno, nambari ambazo hutamkwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili na nyengine hutamkwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza, mfano wa maneno yenye nambari zinazo tamkwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili ni:

7bu ===== Saba ni nambari inayotamkwa kwa Kiswahili.

6ki ===== Sita nimbari inayotamkwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Mku5 ===== Tano ninambariinayo tamkwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Maneno yenye Nambari zinazotamkwa kwa kutumia Lugha ya Kiingereza ni :

2ma ===== two ni nambari yenye kutamkwa kwa lugha ya Kiingereza yenye maana ya mbili.

9t ===== nine ni nambari ambayo hutamkwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza na inawakilisha tisa.

4mu ===== four ni nambari inayotamkwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza na inawakilisha nne.

Pia kuna maneno yenye nambari ambazo hutamkwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza mfano :

Jedwali na. 4.10 Maneno yenye Nambari hutamkwa kwa Kiswahili na Kiingereza

Neno	Kingereza	Kiswahili	Maana ya sentensi
2100	2	100	Tumia
2o8	2	8	Tuonane

Chanzo kotoka Utafiti huu (2018)

Tanbihi:

Nambari 2 kwa Kiingereza hutamkwa two yenye maana ya mbili, na nambari 100 kwa Kiswahili hutamkwa mia kutokana na wazungumzaji wa lugha wanapowasiliana kwa kutumia simu za mkononi wanapotumina ujumbe hutumia nambari hizi kwa kuwasilisha maana ya neno tumia (2100). Na nambari 8 kwa lugha ya Kiswahili hutamkwa nane nambari hii ikitanguliwa nambari mbili, kisha ikafuatiwa na irabu o na kumalizia nambari 8 na huandikwa (2o8) watumiaji wa lugha hutumia kuwasilisha maana ya neno tuonane.

Jedwali na. 4.11: Utumiaji waLugha Tandawazi katika Kiwango cha Sentensi

Neno	Maana ya sentensi
Vp hjmb	Vipi hujambo
Wa2 wote wameu100	Watu wote wameumia
Ni2mie sms	Nitumie ujumbe
Watoto hupelekwa 4ro kila siku ya j5	Watoto hupelekwa forodhani kila siku ya jumaatano
Watahiniwa wamesitishwa kufanya mitihani yao kwa7bu ya pay	Watahiniwa wamesitishwa mitihani yao kwa sababu hawajalipa
Bc usinifuatilie km vp nitakufanyia some thing wrong	Basi usinifuatilie nitakufanyia kitu kibaya
2kopa1	Tiko pamoja
Niko alone	Niko peke yangu
Hayat karume ni rais wa zenji	Marehemu karume ni rais wa Zanzibar
Ni2mie smskunijuulisha	Nitumie ujumbe kunijuulisha
Wanafunzi wa kidato wamemcall mwalimu kuhusiano na mku5 wao wa year	Wanafunzi wa sekondari ya juu wamempigia simu mwalimu wao kwa ajili ya mkutano wao wa mwaka
J3 trh 23 skuli za znz zinafunguliwa baada ya kufungwa kwa7bu ya mvua	Jumaatatu tarehe 23 skuli za Zanzibar zinafunguliwa baada ya kufungwa kwasababu ya mvua
Ok niweight kidogo nakuja	Haya nisubiri kidogo nakuja
Teacher wa Kisw na mmaind	Mwalimu wa Kiswahili na mpenda

Neno	Maana ya sentensi
2o8 baadae kujadili ile problem	Tuonane baadae kwa kujadili lile tatizo
Anahangaika kutafuta solution ya problem lake	Anahangaika kutafuta muafaka wa tatizo alilo nalo
Dk alinishauri kumaliza dose ili kupoa homa inayo nisumbua	Daktari alinishauri kumaliza dawa alizonipangia ili kupoa homa
Alinishtua na kuniambia angalia figer ile	Alinishtua na kuniambia angalia umbo (kiuno) kile
Alizi100 baada ya kupokea trf ya msiba wa bb yake	Alizimia baada ya kupokea taarifa ya msiba wa baba yake
4mu za kujiunga na chuo mara nyng hulipiwa	Fomu za kujiunga na chuo mara nyingi hulipiwa

Chanzo kutoka Utafiti huu (2018)

4.4 Kubainisha Athari za Lugha Tandawazi katika Kiswahili Sanifu

Lengo la pili la Utafiti huu ilikuwa nikubainisha athari za lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu. Watafitiwa wa utafiti huu wamesema kuwa athari ya lugha tandawazi zinazopatikana katika Kiswahili sanifu ni athari ya kiisimu. Masamba (2004) amesema isimu ni taaluma ya ufafanuzi, uchambuzi na uchanganuzi wa lugha kwa kutumia mbinu za kisayansi. Isimu ni sayansi ya lugha (TUKI 1990). Besha nae amesema kuwa isimu ni taaluma ambayo huchunguza na kuweka bayana kanuni ambazo ndizo msingi wa kila lugha. Vile vile Mdee na wenzake (2011) wamesema kuwa Isimu ni taaluma ya kuchunguza sayansi ya lugha. Kutokana na fasili hizi za

wataalamu mbalimbali, mtafiti wa utafiti huu anakubaliana nao kuwa isimu ni taaluma inayochunguza lugha ya mwanaadamu kisayansi.

Kiswahili Sanifu kimeathiriwa na utandawazi kupitia misingi yake ya kiisimu ya lugha na hivyo Kiswahili Sanifu kimeathiriwa kimatam-shi (fonolojia), kimaana (semantikia), kimaumbo ya maneno (mofoloji) na kiupatanisho wa kisarufi (sintaksia).

Jedwali na. 4. 12: Majibu ya Watafitiwa juu ya Athari ya Lugha Tandawazi

Sampuli	Athari za kifonolojia	Athari za semantikia	Athari za Mofolojia	Athari za sintaksia	Jumla
A(30)	10	07	09	02	28
B(20)	06	08	05	01	20
C(10)	03	02	02	02	09
D(10)	02	02	02	02	08
E(10)	03	01	04	02	10
Jumla (80)	24	20	20	09	75

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

4.4.1 Athari ya Lugha Tandawazi kifonolojia (Kimatamshi)

Fonolojia ni utanzu wa isimu unaochunguza jinsi sauti ya lugha mbalimbali ambazo ni mahsusi zinavyotumika, zinavyounganishwa na zinavyo pangwa katika lugha mahsusi ili kuunda, maneno yenye maana (Habwe na Karanja 2004). Nae Chomi (2013) anasema kuwa: fonolojia ni taaluma inayohusisha maelezo ya sauti au vitamkwa vya lugha fulani kama vile Kiswahili. Pia Massamba amesema kuwa

fonolojia ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchunguzi, uchambuzi na uainishaji wa sauti pambanuzi ambazo hutumika katika mifumo mbalimbali ya sauti za lugha za binaadamu . Hivyo lugha tandawazi imeziathiri sauti za lugha ya Kiswahili kimaandishi. Hii ina maana ya kwamba utaratibu utumikao katika uandishi wa sauti za maneno ya lugha hauzingatii utaratibu wa kimaandishi unaokubalika katika lugha. Vitamkwa vya lugha (fonimu) hugawika katika sehemu kuu mbili, ambazo ni konsonanti na irabu. Mara nyingi katika lugha ya Kiswahili, katika kujenga silabi za neno, hutumika konsonanti na irabu au nazali, ili kupata neno lenye maana kamili lakini tunapotumia lugha tandawazi katika mawasiliano yetu hutumia konsonanti tupu, au konsonanti na nazali bila ya kutia irabu kwenye uandishi. Mifano:

Jedwali nambari 4:13: Mifano ya Maneno yaliyodondoshwa Baadhi ya Irabu

Neno/ Tungo	Irabu iliyo Dondoshwa	Maana ya Tungo
Vp hl yk	i,i,a,i, a na o	Vipi hali yako
Utkj lo	a , u a na e	Utakuja leo
Lkn hj	a,i,i a na i	Lakini haji
Wtt wzr	a,o,o a u na i	Watoto wazuri
Asbh njema	u u na i	Asubuhi njema
Ww hujambo	e na e	Wewe hujambo
Ktk hili hayumo	a,i na a	Katika hili hayumo

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

4.4.1.1 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Maneno yaliyodondoshwa Baadhi ya Irabu

Katika tungo zilizooneshwa kwenye jedwali (4.13) hapo juu baadhi ya irabu zimedondoshwa na kubakia konsonanti pekee, konsonanti ambazo zimewakilisha maana ya maneno. Kiuhalisia katika Kiswahili Sanifu wazungumzaji wa lugha hiyo hutumia konsonanti pamoja na irabu katika kuwasilisha silabi zinazojenga maneno yatumikayo katika mawasiliano yao na ndio maana Kiswahili kikawa ni lugha rahisi kujifunza na pia kufahamika kwa wanaowasiliana. Kutokana na utandawazi Kiswahili kimeathirika mno kifonolojia/Kimatamshi na kupelekea hata baadhi ya fonimu kutopewa irabu katika uandishi wa baadhi ya maneno ya mawasiliano ya wazungumzaji.

Pia baadhi ya watafitiwa hutumia vibaya baadhi ya fonimu za Kiswahili kwa mfano fonimu ya ukanushi **si** watumiaji wa lugha tandawazi huandika fonimu ya kingereza **C** na huwa imetosha kwao kutoa maana halisi ya neno. Mfano ufuatao kwenye jedwali ni hoja thabiti:

Jedwali na.4.13 Mifano ya Matumizi ya Fonimu C Mahali pa Fonimu si katika Maandishi

Lugha tandawazi	Maana ya Sentensi
Ctaki maneno yako	sitaki maneno yako
Co zari	sio zari
Citokuja leo	sitokuja leo

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

Vilevile baadhi ya watafitiwa wamekuja na maoni kwamba watumiaji wa lugha tandawazi hutumia nambari ili kuwakilisha baadhi ya fonimu za lugha ya Kiswahili.

Jedwali na. 4.14 Linaloonesha jinsi Nambari zinavyotumika katika kuandika

Maneno ya Lugha Tandawazi

Lugha tandawazi	Lugha ya Kawaida
Ni2mie ujumbe mfupi	Nitumie ujumbe mfupi
Tuonane 4ro	Tuonane Forodhani
Anaishi Saa 10	Anaishi Saateni

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)

Watafitiwa wengi katika lugha tandawazi hutumia vibaya fonimu za lugha ya Kiswahili na kusababisha Kiswahili kupoteza baadhi ya fonimu zake za msingi katika uwasilishaji wa kimaandishi.

4.4.2 Athari za Kisemantiki

Mtafiti wa utafiti huu amebaini kuwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili hutumia lugha tandawazi wakati wanapofanya mawasiliano yao hasa katika kuwasilisha ujumbe kimaandishi.. Mtafiti pia amebaini kuwa kuna baadhi ya watafitiwa huathirika zaidi kimaana pindi wanapotumiwa ujumbe kwa njia ya simu wenye sura ya lugha tandawazi na kuwafanya wakose kuufahamu ujumbe wenyewe.

4.4.2.1 Maana ya Semantiki

Semantiki ni tawi la isimu linalochunguza maana katika lugha (Craystal 1987). Nao Habwe na Karanja (2004): wanasema kuwa semantiki ni utanzu wa isimu

unaochunguza maana katika lugha ya mwanaadamu. Nae Matinde (2011) anasema kuwa semantiki ni taaluma inayochunguza maana katika kiwango cha leksia, kiwango cha tungo au sentensi na kiwango cha usemi au matini. Hivyo semantiki ni tawi la isimu ambalo huchunguza maana za maneno katika lugha husika. Wazungumzaji wa lugha wanapotumia lugha tandawazi katika mawasiliano yao maana ya neno huwa tata na pengine kutokueleweka kabisa. Watafitiwa wa utafiti huu wamesema kuwa mara nyingi wanapotumiwa ujumbe wenye sura ya lugha tandawazi huwa ni shida kufahamu maana ya neno husika.

Wazungumzaji wa lugha wanapowasiliana kimaandishi kwa sura ya lugha tandawazi mawasiliano mara nyingi huwa yana tabu kufahamika. hii inasababishwa na udondoshaji wa irabu, kuchanganya msimbo wa lugha na hata uchanganyaji wa maneno na nambari kwa wakati mmoja. Mfano:

Jedwali na. 4.15: Maana ya (leksimu) yaliyoandikwa katika Mfumo wa Lugha Tandawazi

Lugha Tandawazi	Kiswahili Sanifu
6ki	Sitaki
4mu	Fomu
Co	Sio
Lkn	Lakini

Chanzo kutoka katika utafiti huu (2018)

4.4.2.2 Utambuizi wa Maana ya Mfumo wa Lugha Tandawazi

Utambuizi wa maana ya vipashio vya lugha tandawazi hujitokeza kwenye viwango vya tungo pia. Katika kiwango hiki hali inakuwa mbaya na ngumu zaidi kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:-

Jedwali nambari 4.16: Maana ya (Tungo) zilizoandikwa katika Mfumo wa Lugha Tandawazi

ni2mie sms	nitumie ujumbe
co ww	Sio wewe
j4 mku5	jumanne mkutano
Ktk wkt huu	katika wakati huu

Chanzo Data kutoka katika Uwandani (2018)

4.4.2.2.1 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Utambuizi wa Maana ya Mfumo wa Lugha Tandawazi

Katika neno 6ki neno hili limechanganya nambari na silabi kwenye mfumo wa Kiutandawazi. Kwenye Kiswahili Sanifu watumiaji na wazungumzaji wa lugha huwa kwao ni vigumu kufahamu maana iliyo kusudiwa. Leksimu fomu imechanganya nambari na silabi, nambari ambayo hutamkwa kwa Kiingereza na kuwekwa pamoja na silabi inayo tamkwa kwa Kiswahili na hivyo wazungumzaji hao huchanganya msimbo (Kiswahili na kiingereza). Hivyo huwa ni vigumu kupata maana halisi ya neno hilo kwa wasiokuwa weledi wa lugha tandawazi.

Pia wazungumzaji wa lugha tandawazi katika mawasilano yao kupitia njia ya ujumbe mfupi huwa wanajaribu kudondosha baadhi ya irabu, na hali hii hupelekea uaandishi

wa konsonant pekee katika ujenzi wa silabi. Jambo hili mara nyengine husababisha utata miongoni mwa watumiaji wa lugha tandawazi katika Kiswahili Snifu. Kwa mujibu wa TUKI (2010) Utata ni hali ya neno au tungo moja kwua na maana zaidi ya moja. Matinde (2012) anasema kwamba utata hutokana na neno au sentensi kuwa na maana zaidi ya moja ambazo si wazi. Akitoa mfano wa utata matinde ameelezea utata uliomo kwenye neno mbuzi. Neno mbuzi lina utata kwasababu hatuwezi kujua mtamkaji amekusudia mbuzi gani? Kuna mbuzi mnyama anaefugwa na pia kuna mbuzi kifaa cha kukunia nazi.

Katika mtindo kama huu wazungumzaji wa lugha tandawazi wanapodondosha irabu hupelekea kutoeleweka kwa maana ya neno husika mfano: tuonane *bndn*. Neno *bndn* linaweza kuwa na maana ya bandani na pia lina weza kua na maana ya bondeni. Pia neno *ktk* linaweza kuwa na maana ya katika na pia linaweza kuwa na maana ya kutoka hivyo utata huu unasababishwa na lugha tandawazi hasa wanaowasiliana wanapotumiana ujmba kwa kutumia njia ya simu.

Wazungumzaji wa lugha tandawazi wamekiathiri mno Kiswahili Sanifu hasa katika isimu maana (semantiki) na miongoni mwa athari kubwa inayojitokeza ni ile athari ya kusababisha utata katika Kiswahili Sanifu.

4.4.3 Athari za Kimofolojia

Athari ya kimofolojia ni athari ambazo hujitokeza pale maumbo ya maneno yanapobadili utaratibu wa uundaji wake. Vilevile hii ni athari inayoharibu maumbo ya maneno katika lugha. Katika utafiti huu, watafitiwa wameichagua athari ya kimofolojia mara 20. Idadi hii inamaanisha kuwa Kiswahili kupitia lugha tandawazi

kinaathirika sana katika uundaji wa maneno. Katika uundaji wa viambishi na maneno ya lugha tandawazi uundaji wake huwa haukubaliki katika Kiswahili Sanifu. Uundaji huu unakuwa haufuatui utaratibu sahihi wa uundaji wa maneno. Hatman (1972) anasema kuwa mofolojia ni tawi la sarufi ambalo huchunguza maumbo ya maneno yalivyo sasa pamoja na historia zao. TUKI (1990) wanasema kwamba mofolojia ni tawi la isimu ambalo huchunguza maneno na aina zake.

Kwa hiyo mofolojia ndio tawi la isimu ambalo huchunguza uundaji wa maneno katika lugha. Tunapotumia lugha tandawazi uundaji wa maneno huwa haufuati utaratibu mzuri Uundaji wa maneno uliosahihi hufuata mbinu mbali mbali za Mbinu hizo ni kama vile mbinu ya ukopaji, mbinu ya ufupishaji, mbinu ya uambatanishaj, na mbinu ya uradidi lakini mbinu zote hizi hazifuatwi ipasvyo katika uundaji wa maneno wa lugha tandawazi.

Mfano uundaji wa kiunganishi wa neno lakini ambalo watumiaji wa lugha tandawazi huliwakilisha kiamaandishi kwa (lkn) umetumia mbinu ya ufupishaji; hata hivyo utaratibu uliotumika haukubaliki katika Kiswahili Sanifu kwani mbinu ya ufupishaji, ni mbinu ambayo silabi hudondoshwa au kuachwa kabisa sehemu asilia ya neno. Mfano wa neno baba (ba), Morogoro (Moro) na shemegi (shem).

4.4.4 Athari za Sintaksia

Athari ya sintaksia imechaguliwa mara 09 na watafitwa wa utafiti huu. . sampuli A wameichagua watafitiwa wawili (2), sampuli B ameichagua mtafitiwa mmoja 1, sampuli C wameichagua watafitiwa wawili (2), sampuli D wameichagua watafitiwa (2) na sampuli E watafitiwa wawili (2).

4.4.4.1 Tafsiri ya Matokeo kuhusu Athari za Sintaksia

Athari za sintaksia ni athari ambazo zinaharibu muundo wa lugha kwa kutofuata upatanisho wa kisarufi. Watafitiwa wa utafiti huu wameichagua athari hii kwa sababu watumiaji wa lugha tandawazi hawafuati muundo wa lugha katika mawasiliano yao. Kamusi ya Kiswahili (1990) inaeleza kuwa: Sintaksia ni tawi la sarufi linalo shughulikia uchanganuzi wa mpangilio na uhusiano wa vipashio katika sentensi. Nae Radford (1981) anasema kuwa sintaksia ni taaluma inayojishughulisha na namna maneno yanavyoweza kupangwa pamoja kutoa muundo wa sentensi.

Mara nyingi watumiaji wa lugha tandawazi huwa hawafuati kanuni za lugha na hupelekea kuchanganya misimbo katika mawasiliano yao. Inawezekana wakachanganya Kiswanili na Kiingereza au Kiswahili na Kiarabu, kwa mfano, nitakujibu kwa sms, “niko home na tutaonana morrow.” Sentensi hizi zimechanganywa misimbo, mwanzo zimetumia lugha ya Kiswahili na baadae kumalizia kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Mifano mengine ni “nakwenda masjid,” “uko baid na hayat mzee wangu,” sentensi hizi nazo zimechanganya misimbo zimetumia lugha Kiswahili na lugha ya Kiarabu. Kutokana na kuchanganya misimbo sintaksia ya Kiswahili huatirika kwa sababu huchafuliwa na kutoka kwenye uhalisia wake na hivyo Kiswahili hupoteza sifa ya ukuaji wake.

Vilevile sentensi zinazotumia lugha tandawazi huwa hazifuati utaratibu wa muundo wa lugha ya Kiswahili mfano: “2nakwenda kila skukuu 4ro.” Sentesi hii haikufuata mpangilio wa maneno ulio sahihi kwa sababu sentensi ilitakiwa kuanza nan a maneno kila siku kuu. Vilele katika neno 2nakwenda lilitakiwa liandikwe,

tunakwennda na neno 4ro nalo lilitakiwa kuandikwa Forodhani. Kutokana na hali hii Kiswahili huathirika katika muundo wake wa maneno katika sentensi.

4.5 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizo kusanywa katika utafiti huu ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano na mbinu ya ushuhudiaji. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umezingatia malengo mahsusi ya utafiti utafiti umebainisha chimbuko la lugha tandawazi katika Kiswahili sanifu. Sura inayofuata ni sura ya hitimisho, matokeo na mapendekezo.

SURA YA TANO

HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni ya kumalizia utafiti wenye mada isemayo Chimbuko la Lugha Tandawazi na Athari zake katika Kiswahili sanifu. Sura ya tano inaanza kwa kutoa muhtasari wa utafiti mzima. Baada ya hapo sura imetoa matokeo ambayo yamepatikana katika utafiti huu na mwisho sura imeeleza mchango wa utafiti huu na kutoa mapendekezo yaliotolewa na watafitiwa juu ya lugha tandawazi. Aidha, sura hii inapendekeza maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza chimbuko la lugha tandawazi na athari zake katika Kiswahili Sanifu. Utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa mjini magharibi, kwenye wilaya ya magharibi A na B pamoja na wilaya ya mjini. Utafiti uliwashirikisha watafitiwa 80 ambao waligawika katika sampuli tano (5). Kundi la kwanza lilihusisha wataalamu wa lugha ya Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA. Idadi yao ilikuwa ni thelathini (30). Kundi la pili lilikuwa ni la walimu wa skuli ya sekondari ya Fuoni. Idadi yao walikuwa ni ishirini (20). Watoto wenye umri kati ya miaka kumi na mbili na kumi na nane (12-18), wa kijiji cha Fuoni Kibonde Mzungu walikua kumi (10). Vijana wenye umri kati ya miaka kumi na nane na arobaini walikuwa ni kumi (10). Vijana wote kumi (10) walikuwa ni wanafunzi na walimu wa shule ya Hamamni sekondari. Mwisho ilikuwa sampuli ya wazee kumi (10) wenye umri wa miaka arobaini na kuendelea. .

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu za utafiti za hojaji, mahojiano na mbinu ya ushuhudiaji makini. Data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Mtafiti wa utafiti huu alitumia nadharia kidhi ya mawasiliano, akiwa na lengo la kubadili mtindo wa matamshi wakati wa mawasiliano ya kijamii. Utafiti huu ulikusudia kufanyia kazi malengo mawili ambayo ni kuchunguza chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu na pamoja na kubainisha na kufafanua athari za lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu.

Sura ya kwanza ya utafiti ilielezea taarifa za utangulizi za utafiti huu, sura hiyo ilianza kwa kuelezea utangulizi wa ujumla wa mada ya utafiti. Baada ya hapo sura iliainisha usuli wa tatizo la utafiti. Sura hiyo ya kwanza pia ilielezea tamko la utafiti na ilielezea malengo ya utafiti. Vilevile sura iliainisha maswali ya utafiti na kutaja umuhimu wa utafiti na mwisho wa sura palielezwa mipaka ya utafiti. Sura ya pili ilielezea kazi zilizo fanywa na wataalamu mbalimbali kuhusiana na lugha tandawazi pamoja na kuelezea kiunzi cha nadharia, ambacho kilimuongoza mtafiti wa utafiti huu. Katika sura ya tatu mtafiti alielezea jinsi ya utafiti ulivyo fanyika kwa kuainisha eneo la utafiti, pia sura ilibainisha kundi lengwa pamoja na kuainisha usampulishaji. Vilevile sura hii imefafanua mbinu za kukusanya na kuchambua data jinsi zilivyotumika pamoja na vifaa vilivyo tumika katika utafiti huu.

Sura ya nne imewasilisha na kuchanganua data zilizokusanywa katika utafiti huuna sura ya mwisho ambayo ni sura ya tano ilianza kwa kuainisha muhtasari mzima wa utafiti huu pamoja na kutoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Mwisho

kabisa sura ya tano ilitoa mapendekezo ya utafitina kuonyesha hitimisho la utafiti kwa ujumla.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Kubainisha chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu. Utafiti huu umebaini kuwa chimbuko la lugha tandawazi ni wazungumzaji wa lugha wenyewe ambao katika kuwasiliana kwao hawazingatii sarufi sahihi ya Kiswahili na hutumia lugha isiyo sahihi ambayo haikubaliki katika Kiswahili Sanifu. Wazungumzaji wa lugha tandawazi hutumia mitindo ya kuchanganya misimbo, huchanganya herufi na nambari na pia wanapotumiana ujumbe kwa njia ya simu huwa wanakata maneno na kudondosha irabu. Kundi kubwa linalotumia lugha tandawazi ni kundi la vijana wenye umri wa miaka 18-40 na wafanya kazi. Katika kubainisha athari za lugha tandawazi katika Kiswahili sanifu matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa utumiaji wa lugha tandawazi umeleta athari katika lugha ya Kiswahili, athari ambazo watafitiwa wamezitaja kuwa ni:-

- ❖ Athari za Kifonolojia
- ❖ Athari za Semantiki
- ❖ Athari za Kimofolojia
- ❖ Athari za Sintaksia

5.4 Mchango wa Utafiti

Matokeo yaliopatikana katika utafiti huu yatasaidia katika maendeleo ya ukuaji wa lugha ya Kiswahili kwani utafiti umeainisha chanzo cha lugha tandawazi katika lugha ya Kiswahili na umefafanua athari za lugha tandawazi katika lugha ya Kiswahili. Matumaini ya mtafiti ni kwamba kwa yoyote atakaesoma utafiti huu

atafahamu chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu na athari zake kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo msomaji wa utafiti atakua makini wakati wa mawasiliano yake kijamii katika utumiaji wa lugha tandawazi.

Aidha utafiti huu ni changamoto kwa wanaisimu na vyombo vya kukuza Kiswahili juu ya kuukubali mtindo wa lugha tandawazi au kuukataa kuendelea mtindo huu. Pia utafiti utawaongoza wasomi ambao wana malengo ya kudhibiti matumizi sahihi na fasaha ya lugha ya Kiswahili.

5.5 Mapendekezo

Kwa vile lugha tandawazi inakiathiri Kiswahili sanifu, hivyo mtindo huu unaweza kuibua Kiswahili kisichokua rasmi na sanifu, Kiswahili ambacho hakina utaratibu wa kutumia kanuni za lugha zilizo fasaha na kuweza kupoteza uhalisia wake, kwa hiyo wanafunzi wanaojifunza Kiswahili wanaweza kuandika kwa kutumia mtindo huu ambao wanaweza kufupisha maneno na hata kudondosha irabu wakati wanapoandika kwenye madaftari yao kwa sababu wamezoea kutumia mtindo huu katika mawasiliano yao.

5.6 Mapendekezo kwa Taasisi za kukuza na Kuendeleza Kiswahili

Taasisi zinazokuza na kuendeleza Kiswahili ni vizuri watoe elimu inayohusiana na athari za kutumia lugha tandawazi katika Kiswahili Sanifu. Elimu hiyo itolewe kwa kutumia mbinu mbalimbali za kutolea elimu , mbinu ambazo ni kama kuandaa semina ambazo zitajadili athari za mtindo wa kutumia lugha tandawazi, pia waandae majarida tofauti ,majarida ambayo yataelezea jinsi lugha tandawazi inavyo kiathiri Kiswahili na mwisho watoe vipeperushi mbalimbali vyenye kuonesha jisi gani lugha

tandawazi inavyo kiathiri Kiswahili sanifu ili jamii itambue athari za lugha tandawazi katika lugha ya Kiswahili.

Vilevile tasisi za kukuza na kuendeleza Kiswahili ni vyema zikaamua kunzisha vitengo maalum ambavyo vitashughulikia mitindo mipya ya lugha ambayo huibuka katikajamii. Ili kudhibiti athari za mtindo hiyo kutumika katika Kiswahili sanifu. Kwa hiyo vyombo hivi (BAKITA) na BAKIZA) vikae pamoja kujadili namna ya kudhibiti mitindo ya lugha inayo ibuka katika jamii kwa madhumuni ya kulinda, kuhifadhi na kukiendeleza Kiswahili.

5.7 Mapendekezo kwa watumiaji wa Lugha

Watumiaji wa lugha wajaribu kutumia lugha moja tu katika mawasiliano yao na wasichanganye misimbo ya lugha. Pia waache tabia ya kuchanganya maneno na nambari wakati wanapo tumiana ujumbe na waepuke kufupisha maneno kwa kudondosha irabu ili waoneshe uzalendo wao katika kukilinda na kukihifadhi Kiswahili kibakie kua sanifu.

5.8 Mapendekezo kwa Vyombo vya Mawasiliano

Vyombo vya mawasiliano kama magazeti, redio na hata televisheni ni muhimu kwao kutumia lugha zilizofasaha na pia waepuke kutumia lugha zilizo changanya misimbo kwa madhumuni ya kudumisha matumizi sahihi ya lugha.

5.9 Hitimisho

Sura hii ya tano ndio sura ya mwisho ambayo imkamilisha utafiti huu , utafiti ambao unahusiana na chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili sanifu na athari zake.

MAREJELEO

Al-khatib, M. & Sabbah, E. (2008). "Language Choice in Mobile, Text Masege among Jordanian University Students." In, *SKY Journal of Linguistics*.

Baraza la Kiswahili la Taifa (2004). *Kiswahili na Utandawazi*. Dar es Salaam: BAKITA.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Beerkens (2006). "Globalization." [www.beerkens info/files Globalization pdf](http://www.beerkens.info/files/Globalization.pdf) (2006).

Chomi, W. E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojiaya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Craaystal (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. New York: Oxford University Press.

----- (2008). *Texting. The gr8 db8*. New York: Oxford University Press.

Cozyby, P.C & Bates, S. C. (2012). *Methods in Behavioral Science Research (11thed)*. New York.

Dadi, K.S. (1995). *Dhima ya Vyombo vya Habari katika Matumizi ya Misamiati, katika Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: TUKI.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

- Hatman, R. (1972). *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Applied Science Publishers.
- Idarous, A. S. (2005). "Makosa yanayofanywa Mara kwa Mara katika Matumizi ya Kiswahili," katika *Makala za Semia za Kimataifa ya waandish wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing.
- Kingei, K. & Kobie, C. (2007). "Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng nchini Kenya." Katika Jarida la *Kiswahili* la TUKI.
- Kombo, D. & Tromp, P. (2006). *Proposal and Thesis. Writing an Introduction*, Nairobi Paulines Publication Africa.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology and Techniques*. New Delhi: New Age Internation Publishers.
- Kress, T. M. (2008). *Criticalprexis Research: Breathing New Life into Research Methods for Teachers*. United State of America.
- Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M. & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Masamba, D (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Daresalaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2011). *Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.

- Masamba D. P. B., Msanjila, Y. P. & Kihore, Y. M. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee na Wenzake (2011). *Kamusi ya Karne ya 21: Kamusi ya Kiswahili yenye Uketo Zaidi katika karne hii*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Matinde, R. S. (2014). *Dafina ya Lugha. Isimu na Nadharia, Sekondari Vyuvo vya kati na Vyuvo Vikuu*, Mwanza, Serengeti Educational Publisher.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uihakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.
- Mphahlele, M and Mashamaite, K. (2005). "The Impact of Short Message Service (sms). Language and Language Proficiency of Learners and the sms: A challenge for Educators and Lexicographers." In *the African Journal of Languages Vol. 13, pp 34-46*.
- Mutembei, A. (2011). "Kukitandawazisha Kiswahili kupitia Simu za Kiganjani: Tafakari kuhusu Isimu Jamii."
- Nkwera, F. (1979). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuvo*. Dares salaam Tanzania Publishing House.
- Ongonda, N. A. (2011). *Sytactic Aspects in Text Messaging*. World Journal of English Language.
- Radford, A. (1981). *Transformational Syntax*. Cambridge University Press.
- Sigh. K. (2007). *Quantitive Social Research Methods*. India Sage Publication.

TUKI (1990). *Kamusi ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI (2010). *English Kiswahili Dictionary*. Dar es Salaam: TUKI.

Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basics*. London: Routledge Taylor and Francis Group.

Wamitilia, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

KIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO NAMBA 1: HOJAJI KWA WATAALAMU WA LUGHA

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII

Utafiti huu unahusu chimbuko la lugha tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu .Tafadhali jibu maswali haya kwa kiasi ya unavyo ya fahamu ili usaidie katika kutoa taarifa sahihi ambazo zitapelekea kupata taarifa yakinifu yatakayo chochea kukua na kuenea kwa Kiswahili.Majibu ya maswali ya utafiti huu ni siri ya mtafiti na mtafitiwa .

Umri -----, jinsia-----, kazi -----elimu-----.

1. Jee, Lugha tandawazi imeanza na watumiaji wa simu,wazungumzaji wa lugha au taasisi za kielimu.?

Jee, unapowasiliana kwa njia ya simu mara nyingi huwa unapig / unapigiwa, unaandika/ unaandikiwa ujumbe au yote mawili (kupiga au kuandika).?

2. katika mawasiliano yako jee, unachanganya lugha mbili kwa wakati mmoja ?

3. Kama ndio toa mifano ya maneno ambayo unapenda kutumia .

jee, unapoandika ujumbe katika simu unachanganya herufi na nambari ?

b. Ikiwa ndio toa mifano,

4. jee,katika mazungumzo yako umeshawahi kuchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja ?

-----.

b) Kama ndio toa mifano ya maneno ,

-----.

5. Unapo changanya lugha mbili kwa wakati mmoja jee, hua mnafahamiana kaatika mazungumzo?

-----.

6. Toa maoni yako juu ya -:

a- kuchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja ,

-----.

b- kuchanganya herufi na maneno,

-----.

7. kama mtindo wa kuchanganya lugha utaendelea , unahisi Kiswahili kitakuwa katika nafasi gani baadae?

-----.

8. Andika mifano ya maneno ambayo -:

a. yamechanganywa lugha mbili kwa pamoja.

-----.

b. huchanganya herufi na nambari,

9. Ikiwa unayo unayo maelezo ya ziada andika hapa chini.

-----.

AHSANTE KWA MASHIRIKIANO YAKO

Kiambatanisho namba 2 Dodoso kwa Wazungumzaji wa Lugha

1 Unapoandika ujumbe katika simu hua unatumia mtindo wa kuchanganya herufi na nambari?

-----.

2 Jee, wakati unapozungumza hua unachanganya lugha mbili kwa wakati mmoja?

-----.

3 mtindo wa kuchanganya lugha mbili unadhani unaleta athari gani katika lugha ya kiswahili?

-----.

4 toa ushauri wako kwa :

a- Watumiaji wa kiswahili.

-----.

b- Vyombo vya mawasiliano.

-----.

c- Taasisi za kukuza na kuendeleza kiswahil.

-----.

5 toa maoni yako kuhusu kutumia mtindo wa kuchanganya lugha mbili kwa wakati mmoja .

-----.

b- kuchanganya herufi na nambari.

6- unafikiria nini kuhusian na Kiswahili cha baadae?

AHSANTE KWA MASHIRIKIANO YAKO